**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# Tamko la Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb) Kuhusu Utoaji wa Huduma za VVU na UKIMWI kwa Makundi Maalum yaliyo katika Hatari zaidi ya maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI nchini Tanzania, 16 Februari 2017

Kwa mujibu wa utafiti wa viashiria vya UKIMWI na Malaria nchini wa mwaka 2011/12, wastani wa kiwango cha maambukizi ya VVU miongoni mwa watu wenye umri kati ya miaka 15 - 49 ni asilimia 5.1 (5.1%) Hii inamaanisha kuwa katika kila watu 100, watu 5 wanaishi na maambukizi ya VVU. Aidha, inakadiriwa kuwa takribani watu 1,325,271 wanaishi na VVU. Kati yao, watu 839,574 wanapata dawa za kudumaza VVU katika vituo 4,737 vinavyotoa huduma hii katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa mujibu wa takwimu kwa kipindi kinachoishia Juni 2016.

Tafiti pia zinaonyesha kuwa hali ya maambukizi ya VVU kwa makundi maalum yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi iko juu ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa 5.1%. Maambukizi kwa makundi haya ni kama ifuatavyo:- miongoni mwa watu wanaotumia madawa ya kulevya kwa kujidunga sindano ni asilimia 36, wanawake wanaofanya biashara ya ngono ni asilimia 26, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao ni asilimia 25, na wasichana wadogo wa umri balehe miaka 15 -19 (1.1%), wasichana wa umri kati ya miaka 20 - 24 ni asilimia (4.4%), ikilinganishwa

na watoto wa kiume wenye umri huo huo ambao viwango vya maambukizi ni 0.6% na 2.8%. Hali hii ilisababisha Serikali kupitisha **Mwongozo wa Huduma za VVU na UKIMWI kwa Makundi Maalumu wa mwaka 2014**.

Pamoja na nia njema ya Serikali na wadau wa ndani na nje ya nchi katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kuanza utekelezaji wa huduma za VVU na UKIMWI kwa kutumia mwongozo huo katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya (Vituo vya Afya na Zahanati), tulibaini kuwa **kumekuwa na matumizi mabaya ya miongozo ya Serikali ya kupambana na VVU na UKIMWI katika maeneo mbali mbali hapa nchini.**

Uchunguzi uliofanywa na kikosi kazi maalumu cha Serikali cha kufuatilia uwezekano wa kuwepo kwa shughuli za kuraghibisha (promotion) mahusiano ya ki-ngono ya jinsia moja **ulibaini ya kuwa**, mbali na kufanya shughuli za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, **baadhi ya wabia walikuwa wakifanya shughuli za uraghibishi (promotion) wa vitendo vya mapenzi ya jinsia moja, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria za nchi**. Serikali imeweza kupata ushahidi wa kina kuhusu uwepo wa hali hiyo.

Hali hii, ilisababisha Wizara yangu kutoa tamko mnamo tarehe **25 Oktoba, 2016** kuhusiana na hali ya utoaji huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalum yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi ya VVU, ambapo pamoja na mambo mengine nilisitisha kwa muda utoaji wa huduma za VVU na UKIMWI katika ngazi ya jamii ili;-

i. kuruhusu kufanyika kwa mapitio ya mwongozo wa Taifa wa utoaji wa huduma hizo kwa makundi maalum,
ii. kuangalia upya jinsi ya kuwapanga wadau mbali mbali katika ngazi ya Mkoa/Halmashauri, na

iii. kufanya mapitio katika malengo ya utekelezaji katika Mikoa husika pamoja na kuandaa na kuhuisha mitaala ya kufundishia utoaji wa huduma hizo katika ngazi ya jamii.

Tangu tamko hilo lilipotolewa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kushirikiana na wadau wote katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI imeweza kufanya yafuatayo:

- Kiliundwa kikosi kazi cha kufanya mapitio ya Mwongozo wa Huduma za VVU na UKIMWI kwa Makundi Maalum wa mwaka 2014 na mitaala na kuandaliwa hadidu za rejea ambazo zimeongoza zoezi zima la kufanya mapitio ya mwongozo huo na kuja na toleo la pili la **Mwongozo wa Huduma za VVU na UKIMWI kwa Makundi Maalumu la mwaka 2017**. Kikosikazi hiki cha wataalam na wadau wa huduma za VVU na UKIMWI kilihusisha wawakilishi kutoka asasi mbalimbali za Serikali, mashirika ya kigeni, wahisani na mashirika ya kiraia na kilikutana kuanzia tarehe 28/10/2016 hadi 7/12/2016.

- Kuandaa mitaala ya mafunzo na bango kitita kwa ajili ya huduma kwa makundi maalum ngazi ya jamii.

- Wizara inaendelea kumalizia kazi ya kuandaa mitaala ya mafunzo ya huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalumu na kazi hii itamalizika kabla ya mwisho wa mwezi Februari 2017. Huduma za jamii kwa makundi maalum zitaendelea kutolewa kwa kuzingatia mitaala hiyo kwa kupitia zahanati na vituo vya Afya mbali mbali hapa nchini.

- Aidha, suala la wabia/wadau kugawana maeneo ya kufanyia kazi kwa kugawana Kata miongoni mwa wabia wawili au zaidi limefanyiwa

mapitio na kukubaliana kwamba, **kila mbia atafanya kazi zote za huduma kwa makundi maalum katika Mkoa/Halmashauri bila kuingiliwa na mbia/mdau mwingine.** Utekelezaji wa jambo hili utafanyiwa usimamizi wa karibu na timu za uendeshaji huduma za afya za Mikoa (RHMT) na zile za Halmashauri (CHMT) husika.

- Vilevile, kikaokazi cha Makatibu Wakuu wa Wizara saba (Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Ofisi ya W aziri Mkuu, Katiba na Sheria; Mambo ya Ndani ya Nchi; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na Viwanda na Biashara) ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusika katika shughuli zinazoyagusa makundi hayo kimekuwa kinakutana ili kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora na sahihi ya utoaji wa huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalum bila ya kuathiri sheria za nchi.

**Kwa tamko hili ninalolitoa leo tarehe 16 Februari, 2017 naagiza yafuatayo:**

1. Huduma za kupambana na VVU na UKIMWI katika makundi haya maalum zitatolewa kwa **kufuata Mwongozo (uliopitiwa) wa utoaji huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalum wa mwaka 2017 na bila kukiuka Sheria na taratibu za nchi.**

2. Huduma za kupambana na VVU na UKIMWI katika makundi haya maalum zitaendelea kutolewa katika vituo vya kutolea **huduma za Afya, hususan katika zahanati na vituo vya afya vitakavyoteuliwa na kuwezeshwa kutoa huduma stahiki kulingana na mahitaji ya jamii.** Mfumo huu unaendana na mwongozo uliopitiwa wa utoaji huduma za VVU/UKIMWI kwa makundi maalum wa mwaka 2017 na

mwongozo wa huduma za tiba na matunzo kwa wanaoishi na VVU (WAVIU) wa mwaka 2017. **Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha watumishi wanapatiwa mafunzo ya ziada katika utoaji huduma rafiki kwa makundi maalum.** Huduma zitakazotolewa ni pamoja na huduma za kitabibu (Bio-medical Interventions), huduma za mabadiliko ya kitabia (Behavioural Interventions) na huduma za kuwajengea utengamano na za kiuchumi (Structural and Income Generation Interventions).

3. Ninaagiza mamlaka zote za utoaji huduma za afya kuhakikisha kuwa **huduma za VVU na UKIMWI zinapatikana kwa mtu yoyote nchini bila ubaguzi wa aina yoyote** kwa kuwa ubaguzi katika utoaji wa huduma za afya nchini ni kinyume cha sharia, sera na taratibu za nchi. Aidha, Serikali inasisitiza kuwa huduma za afya ikiwemo huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalumu bado zinaendelea kutolewa bila malipo kwa wahitaji wote bila ubaguzi au unyanyapaa, na endapo mtu yeyote hususan katika makundi maalum haya atakosa huduma asisite kutoa taarifa kwa Mganga Mkuu wa Halmashauri husika, Mganga Mkuu wa Mkoa na Wizara ya Afya kupitia kitengo cha mawasiliano. Namba maalum zitatolewa kwa ajili ya huduma hiyo.

4. Utaratibu wa awali wa kutoa huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi maalum kwa **kutumia vituo maalum (Drop in Centers**) **hautatumika tena**. Na pale itakapolazimu, huduma mkoba (outreach services) kwa kutumia watoa huduma za afya itatolewa. Kwa tamko hili, Wizara ya Afya haitatambua vituo hivi maalum vya kutoa huduma za VVU/UKIMWI kwa makundi maalum zaidi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa kisheria.

5. Aidha, ninaagiza kuwa, mamlaka za usajili na usimamizi wa asasi zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za afya **kusimamia kwa ukamilifu usajili wa asasi** hizi kulingana na sheria za nchi na kuhakikisha asasi zinatoa ripoti za utekelezaji wa shughuli zao na za fedha (ikiwemo kubainisha wazi vyanzo vyao vya fedha) kulingana na sheria na taratibu za nchi kama zilivyoainishwa na mamlaka ya usajili wa asasi zisizo za kiserikali (NGO’s).

6. Wabia wa kutoa huduma za VVU na UKIMWI katika makundi maalum wanapaswa **kuzingatia maeneo waliyopangiwa kufanya kazi** kulingana na barua itakayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Ninawaagiza Watendaji Wakuu wa Mikoa, Wilaya (Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri) kufuatilia kwa karibu shughuli zote zinazofanywa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayotoa huduma za VVU na UKIMWI katika maeneo yao.

7. Vikaokazi vya Makatibu Wakuu wa Wizara za: (Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; OR-TAMISEMI; Ofisi ya Waziri Mkuu, Katiba na Sheria; Mambo ya Ndani ya Nchi; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na Viwanda na Biashara) ambavyo kwa namna moja au nyingine vinahusika katika shughuli za makundi haya, vitaendelea kufanyika mara kwa mara ili kupata mrejesho wa jinsi huduma hizi zinavyoendelea kutolewa nchini. Iwapo Serikali itabaini ukiukwaji wa utoaji wa huduma kwa mujibu wa miongozo, sheria na taratibu za nchi, au iwapo kutakuwa na malalamiko kutoka ngazi ya Jamii, basi **Kamati hii ya Makatibu Wakuu ndiyo itakayotakiwa kulishughulikia suala hilo kwa kupitia vyombo vyake husika, na sio Wizara ya Afya, pekee.** Na endapo kutakuwa

na jambo lolote la kisera kuhusu utoaji huduma za VVU na UKIMWI kwa jamii, Kamati hii ya Makatibu Wakuu ndio itakamyoshauri Waziri wa Afya juu ya hatua za kuchukua.

**HITIMISHO**

Maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa makundi maalum nchini Tanzania yapo juu sana kulinganisha na wastani wa kiwango cha maambuzi nchi nzima. Ili kupunguza maambukizi ya VVU nchini, na kuweza kuchangia kutokomeza UKIMWI duniani ifikapo mwaka 2030, ni dhahiri kuwa tunao wajibu wa kuweka mipango na mikakati ya kupambana na VVU na UKIMWI kwa makundi haya. Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa wadau wote katika mapambano dhidi ya UKIMWI hususan wale wanaojishughulisha na utoaji huduma katika makundi maalum **kufuata miongozo, mitaala na ushauri unaotolewa na Serikali katika kufanya shughuli zao na kuhakikisha hawakinzani na Sheria za nchi zilizowekwa ikiwemo sheria inayokataza kuraghibisha vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.**

Aidha, ninawataka wadau wote kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zote zinazofanyika katika ngazi husika (Kamati za Usimamizi wa Huduma za Afya za Halmashauri na Mikoa) kwa wakati ili kuiwezesha Serikali katika ngazi zote kufuatilia kwa karibu namna nchi yetu inavyopiga hatua katika kutokomeza janga la UKIMWI.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**